



*Namba ya Whatsap: 0752965019/ +255 757 411 482*

# KUNENA KWA LUGHA,MIUJIZA,MAONO, KUTOA UNABII

Kunena kwa lugha, miujiza, maono na kutoa unabii husemwa kuwa ni "karama za Roho Mtakatifu":*"Lakini kila mmoja hupewa ufunuo wa Roho kwa kufaidiana. Maana mtu mmoja hupewa kwa Roho neno la hekima; na mwingine neno la maarifa, apate kulingana na Roho yule yule; mwingine imani katika Roho yeye yule; na mwingine karama za kuponya katika Roho yule mmoja; mwingine matendo ya miujiza; mwingine unabii; mwingine kupambanua roho; mwingine aina za lugha; na mwingine tafsiri ya lugha; lakini kazi hizi zote huzitenda Roho huyo mmoja, yeye yeye, akimgawia kila mtu peke yake kama apendavyo yeye."*(1 Wakorintho 12:7-11)

Maonyesho haya mbalimbali, hasa kunena kwa lugha na kuponya, yamekuwa maarufu sana siku hizi kwa sababu ya dhehebu moja la Kikristo linaloitwa Kanisa la Kipentekoste. Kanisa hili lilianza miaka ya 1890 na lilijengwa juu ya uzoefu wa wanafunzi wa kanisa la kwanza katika siku ya Pentekoste. Lakini hakuna onyesho la kunena kwa lugha wala miujiza lililotokea kanisani kwa zaidi ya miaka elfu moja na mia tisa. Hebu tuone Biblia inasema nini kwetu.

**✦✦✦Kunena kwa Lugha✦✦✦**

Onyesho hili la Roho Mtakatifu lilihusisha kunena kwa lugha mbalimbali; lilianza siku ya Pentekoste:*"Wote wakajazwa Roho Mtakatifu, wakaanza kunena kwa lugha nyingine, kama Roho alivyowajalia kutamka."*(Matendo 2:4)

Uwezo huu wa kunena kwa lugha ulitolewa kwa waumini wengine baadaye wakati mtume "aliweka mikono yake juu yao":*(Matendo 19:6)*

Lakini Paulo alieleza wazi kuwa masharti maalum yalipaswa kutimizwa ikiwa kunena kwa lugha kungetokea wakati wa mkutano wa ibada:

*"Kama mtu akinena kwa lugha, wanene wawili au watatu, si zaidi, tena zamu kwa zamu, na mmoja na afasiri. Lakini asipokuwapo mwenye kufasiri na anyamaze katika kanisa; aseme na nafsi yake tena na Mungu.."* (1 Wakorintho 14:27,28)

Paulo alisema wazi kuwa "wawili au watatu si zaidi" wanapaswa kunena, na kwa "zamu," yaani mmoja baada ya mwingine. Aidha, alisema kuwa "lazima mtu mmoja atafsiri." Hali hii ilikuwa ya lazima kiasi kwamba mtume aliamuru kuwa "ikiwa hakuna mfasiri, na anyamaze katika kanisa." Masharti haya ya muhimu kabisa yamepuuzwa na makanisa ya Kipentekoste siku hizi.

Lengo la "kunena kwa lugha" katika kanisa la kwanza lilikuwa ni lipi? Paulo aliandika:

*"Sasa, ndugu, nikija kwenu na kunena kwa lugha, nitawafaidia nini, nisipowahutubia kwa ufunuo, au kwa maarifa, au kwa unabii, au kwa mafundisho? … Imekuwaje, basi, ndugu? Mnapokutanika, kila mmoja ana*

*zaburi, ana mafundisho, ana ufunuo, ana lugha, ana tafsiri. Yote na yafanyike kwa kujenga."*(1 Wakorintho 14:6,26)

Kunena kwa lugha kulikuwa ni kwa ajili ya kutoa ufunuo wa Kimungu ili kulijenga kanisa kiroho kupitia maneno na ujumbe kutoka kwa Mungu — katika kipindi ambacho Agano Jipya lilikuwa bado halijaandikwa.

Mtume Paulo anaendelea kusema: *"Maana yeye anenaye kwa lugha hasemi na watu, bali husema na Mungu; kwa maana hakuna asikiaye; lakini husema mambo ya siri kwa roho yake."*(1 Wakorintho 14:2)

Maneno haya hutumiwa kusema kuwa wale wanaonena kwa lugha hunena maneno ambayo Mungu peke yake ndiye anayeyaelewa. Hivyo, bidii kubwa ya wengine kunena kwa "lugha" kila wakati huonekana kama ibada ya kumwelekea Mungu. Lakini si hivyo Paulo alivyofundisha. Alisema kwamba anayenena kwa lugha hunena katika lugha isiyojulikana, *"hakuna asikiaye; lakini husema mambo ya siri."* Hii ndiyo ingekuwa hali kama mtu angesema Kichina au Kijapani kwa kundi la watu wanaojua Kiingereza tu. Wasikilizaji wasingeweza kuelewa hata neno moja. Wakijiuliza kinachosemwa, wangesema: "Mungu peke yake anajua."

Katika hali kama hiyo ya "lugha isiyojulikana," ni kweli kusema kuwa mnenaji *"hasemi na watu, bali na Mungu,"* kwa sababu ni Mungu tu anayeweza kuelewa.

Kunena kwa lugha zisizoeleweka na wasikilizaji hulifanya jambo hilo kuwa fumbo, kwa kuwa maneno hayaeleweki. Uwezo huu ulikuwa ishara kwa wasioamini: *"Basi lugha ni ishara, si kwa wale waaminio, bali kwa wale wasioamini; bali unabii ni kwa wale waaminio, si kwa wasioamini."* (1 Wakorintho 14:22)

Hivyo basi, kunena kwa lugha kulikuwa ni ishara kwa wasioamini. Lakini leo hii hali imekuwa kinyume chake; kunena kwa lugha kumegeuka kuwa ishara kwa waumini. Lakini haikuwa hivyo katika kanisa la kwanza, kama tunavyosoma:*"Imewezekanaje basi sisi kusikia kila mtu katika lugha ya asili ya nchi tulikozaliwa? Wakashangaa wote, wakashikwa na shaka, wakiambiana, Maana yake nini haya?"* (Matendo 2:8,12)

Jambo hili liliwashangaza wasioamini, na lilikuwa onyesho kuu kwao la nguvu za Mungu.

Mtume Paulo alinena kwa "lugha" nyingi zaidi ya wote: *"Namshukuru Mungu, ya kuwa nanena kwa lugha kuliko ninyi nyote."* (1 Wakorintho 14:18)

Alinena kwa "lugha" nyingi kwa kuwa alikuwa mtume maalum kwa mataifa:
*"Maana yeye aliyefanya kazi ya mitume kwa Petro kwa ajili ya wale waliotahiriwa, ndiye aliyenifanya mimi niwe mtume kwa ajili ya Mataifa."* (Wagalatia 2:8)

Hata hivyo, katika mikutano ya kanisa kati ya waumini, mtume Paulo aliikataza matumizi ya karama hii ikiwa hakuna yeyote wa kuielewa lugha hiyo: *"Isipokuwa kama mtatoa maneno yanayoeleweka kwa ulimi wenu, watu watajuaje mnayosema? Mtakuwa mkinena hewani tu. … Basi kanisa lote likutanikapo pamoja, na wote wakanena kwa lugha, kisha wakaingia watu wasiojua neno au wasioamini, je! Hawatasema ya kuwa mmechanganyikiwa?"*(1 Wakorintho 14:9,23)

Mtume Paulo alisema kuwa kukusanyika na kunena kwa "lugha" haipaswi kufanywa kabisa: *"Kwa maana Mungu si Mungu wa machafuko, bali wa amani. Kama ilivyo katika makanisa yote ya watakatifu."*(1 Wakorintho 14:33)

Na mwenye hekima aliandika vivyo hivyo: *"Uwe na tahadhari na hatua zako uendapo nyumbani kwa Mungu, na ukaribie kusikia kuliko kutoa sadaka ya wapumbavu … Msiwe wepesi kwa vinywa vyenu, wala moyo wako usiwe na haraka kutamka neno mbele za Mungu."*(Mhubiri 5:1,2)

Mtu lazima awe na tahadhari mbele za Mungu. Kunena kwa lugha kwa wakati mmoja na watu wengi hakumnufaishi yeyote.

Angalia kinachosemwa juu ya karama hii ya lugha:*"Kuna lugha, zitakoma."*(1 Wakorintho 13:8)

Paulo alisema kuwa uwezo huu au "ufunuo" wa Roho Mtakatifu ungefikia mwisho na kusitishwa kabisa. Hii ni kwa sababu "karama" hii ya Roho Mtakatifu ilikuwa inaweza kuhamishiwa kwa mwingine tu kupitia kwa mtume: *"Petro alipokuwa katika kusema maneno haya, Roho Mtakatifu akawashukia wote waliolisikia neno … kwa maana waliwasikia wakisema kwa lugha, na kumtukuza Mungu."*(Matendo 10:44,46)

Kwa kuwa mitume wote walikufa, basi "karama" hii ya Roho Mtakatifu ilikoma pia.

Kwa nini basi karama hii ya kunena kwa lugha ilitolewa kwa kanisa la mwanzo tu? Ilikuwa ni kwa ajili ya kulijenga kanisa la awali lililokuwa bado changa, kwa ajili ya kutimiza madhumuni mawili:

1. **Ilitimiza agizo kuu la Bwana:***"Basi, enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi."*(Mathayo 28:19) Ilikuwa muhimu kuhubiri Injili kwa mataifa yote kwa lugha inayojulikana na watu, lakini mitume na wanafunzi walijua Kiebrania na Kiaramu tu.

2. **Kunena kwa lugha** kulitumiwa na Mungu kuwasilisha ufunuo wa Kimungu kwa ajili ya kuwaongoza waumini wa

kanisa la kwanza katika kipindi ambacho Agano Jipya lilikuwa bado halijaandikwa: *"Basi, ndugu, nikija kwenu na kunena kwa lugha, nitawafaidia nini, nisipowahutubia kwa ufunuo, au kwa maarifa, au kwa unabii, au kwa mafundisho?"* (1 Wakorintho 14:6)

Sasa je, tutasemaje juu ya "kunena kwa lugha" siku hizi? Tafakari kwa makini hoja hizi:

• Inawezekanaje "karama" iliyokuwa ikipitishwa tu kwa kuwekwa mikono na mtume, ijitokeze tena ghafla baada ya miaka mingi?
• Kwa nini "lugha" hunenwa leo bila mfasiri, kinyume na 1Wakorintho 14:28?
• Kwa nini wengi hunena kwa wakati mmoja badala ya "kila mmoja kwa zamu" kama inavyoelekezwa katika 1 Wakorintho 14:27?
• Kwa nini "lugha" za leo si ishara kwa wasioamini kama ilivyokuwa Pentekoste (Matendo 2:7,8)?

Mafundisho ya wale wanaonena kwa "lugha" leo hii hayafuati mafundisho ya Biblia kulingana na *"Imani iliyo takatifu sana."* (Yuda 1:20)



**✦✦✦Miujiza na Uponyaji✦✦✦**

Hii ni kazi ya "nguvu" ya Mungu kuponya magonjwa ya mwili na ya akili, kuwakomboa watu waliopagawa na

pepo, na hata mara chache, kuwaamsha waliokufa. Karama hii ya Roho Mtakatifu ilitumika katika kanisa la mwanzo kupitia kwa mitume na wanafunzi. Hapa kuna mifano:

*"Wakawaleta wagonjwa hata mitaani, wakawalaza juu ya vitanda na machela, ili Petro akipita, kivuli chake kiwapate baadhi yao … na wale walioteshwa na pepo wachafu, wote waliponywa."* (Matendo 5:15,16)

*"Na Stefano, akiwa amejaa neema na uwezo, alikuwa akifanya maajabu makubwa na ishara miongoni mwa watu."* (Matendo 6:8)

*"Petro akawatoa nje wote, akaingia, akapiga magoti, akaomba; akamgeukia yule mwanamke akasema, Tabitha, inuka. Naye akafumbua macho yake, na alipomwona Petro aliketi."* (Matendo 9:40)

*"Mungu alifanya miujiza ya ajabu kwa mikono ya Paulo … magonjwa yao yakawaondoka, pepo wachafu wakawatoka."* (Matendo 19:11,12)

Miujiza na uponyaji huu wote ulikuwa ni kwa ajili ya wasioamini, kamwe si kwa ajili ya waumini wenyewe. Wakati Timotheo alipokuwa na tatizo la tumbo, Paulo hakumponya. Badala yake aliandika: *"Usinywe maji tu, bali tumia divai kidogo kwa ajili ya tumbo lako, na magonjwa yako ya mara kwa mara."* (1 Timotheo 5:23)

Paulo alishauri Timotheo kutumia divai kidogo kama dawa, lakini hakumwekea mikono ili kumponya.

Siku hizi, Wakristo wengi wenye matatizo ya kiafya hutafuta uponyaji wa miujiza na haijalishi utatokea kwa njia gani. Hali ilikuwa tofauti kabisa katika kanisa la kwanza. Wakristo wa wakati huo walitambua kuwa "nguvu" ya kutenda miujiza ilikuwa ni "ishara" kwa wasioamini tu, na si kwa ajili yao wenyewe. Kusudi la miujiza na uponyaji wa leo ni tofauti kabisa na ule wa nyakati za mitume.

Kuna matukio mawili ambapo mitume wawili waliwafufua watu waliokuwa wamekufa. Tukio hili lilifanywa na mtume Petro:

*"Na huko Yopa palikuwa na mwanafunzi mmoja mwanamke jina lake Tabitha, tafsiri yake ndiyo Dorkasi; mwanamke huyu alikuwa amejaa matendo mema na sadaka alizozitoa. Ikawa siku zile akaugua, akafa; na walipokwisha kumwosha, wakamweka katika chumba cha juu. Na Lida ilikuwa karibu na Yopa; wanafunzi waliposikia ya kwamba Petro yumo Lida, wakatuma watu wawili kwake, wakimsihi, Usikawie kuja mpaka kwetu. Petro akaondoka akafuatana nao. Alipofika wakampeleka katika chumba cha juu; na hao wajane wakamzunguka, wakilia, wakimuonyesha majoho na mavazi, aliyoyafanya Dorkasi alipokuwa pamoja nao. Petro akawatoa wote nje, akapiga magoti, akaomba; akamgeukia yule maiti, akasema, Tabitha, inuka. Naye akafumbua macho yake; hata alipomwona Petro aliketi. Akampa mkono, akamwinua; akawaita watakatifu na hao wajane, akamweka mbele yao yu hai. Habari hii ikajulikana katika Yopa yote; watu wengi wakamwamini Bwana." (Matendo 9:36-42)*

Tukio hili lingine lilifanywa na mtume Paulo:

*"Na kijana mmoja, jina lake Eutiko, alikuwa ameketi dirishani, akalemewa na usingizi mwingi; na Paulo alipokuwa akizidi kusema, usingizi ukamshinda; akaanguka toka orofa ya tatu chini, akainuliwa amekufa. Paulo akashuka, akaangukia juu yake, akamkumbatia, akasema, Msifanye ghasia, maana roho yake imo ndani yake. Kisha akapaa juu, akamega mkate, akala, akaendelea kuzungumza nao sana hata alfajiri, akaenda zake. Wakamtwaa yule kijana yu hai, wakafarijika sana."(Matendo 20:9-12)*

Miujiza yote hii ilifanyika ili kuthibitisha nguvu na utukufu wa Bwana na ujumbe wa injili kwa wale waliokuwa wakialikwa kuteseka na kuchukua msalaba wao na kumfuata Bwana wao. Lakini miujiza yenyewe haikupaswa kuwa msingi wa mtu kuamini au kuwa mfuasi wa Yesu. Bwana mwenyewe hakuwataka watu wa namna hiyo wawe wanafunzi wake:

*"Basi alipokuwa Yerusalemu wakati wa Pasaka, katika sikukuu, watu wengi walimwamini jina lake, walipoziona ishara alizozifanya. Lakini Yesu mwenyewe hakuwaamini wao, kwa sababu aliwajua wote, wala hakuwa na haja ya mtu kumshuhudia habari za mtu ye yote, maana yeye mwenyewe alijua yaliyo ndani ya mtu."(Yohana 2:23-25)*

Imani hii "iliyotegemea miujiza" ilikuwepo kwa wingi katika siku za Yesu, na inaendelea kwa wingi hata leo. Lakini hiyo haipaswi kuwa msingi wa maisha ya Mkristo:*"(Kwa maana) twaenenda kwa imani, si kwa kuona."*(2 Wakorintho 5:7)

Bwana mwenyewe alinena juu ya Wakristo wanaotafuta miujiza katika unabii:*"Wengi wataniambia siku ile, Bwana, Bwana, hatukufanya unabii kwa jina lako, na kwa jina lako kutoa pepo, na kwa jina lako kufanya miujiza mingi? Ndipo nitawaambia wazi, Sikuwajua ninyi kamwe; ondokeni kwangu, ninyi mtendao maovu."*(Mathayo 7:22,23)

Bwana anaelezea jinsi Wakristo wengi *"siku ile"* au siku ya hukumu, watakavyodai kuwa walifanya miujiza mikubwa kwa jina la Yesu Kristo, lakini Bwana mwenyewe atasema: *"Sikuwajua ninyi kamwe… ninyi mtendao maovu."* Bwana atawakataa watendao miujiza hao; anawaita *"watendao maovu."* Yesu hatambui miujiza hiyo kuwa ni yake, wala hawatambui Wakristo hao kuwa ni watumishi wake. Hii ni kwa sababu miujiza hiyo, hata kama inafanywa *"kwa jina la Yesu,"* haikuidhinishwa na Yesu mwenyewe.

Linganisha miujiza iliyofanywa katika nyakati za Yesu na ile inayofanywa leo. Wakati mmoja Yohana alimwambia Yesu: *"Mwalimu, tulimwona mtu mmoja akitoa pepo kwa jina lako, naye hatufuatani nasi, tukamkataza, kwa sababu hafuatani nasi. Yesu akasema, Msimkataze; kwa maana hakuna mtu atakayefanya muujiza kwa jina langu aweze mara kuzungumza vibaya juu yangu."*(Marko 9:38,39)

Mtu huyo aliyekuwa akifanya miujiza hakuwa mmoja wa wanafunzi, wala hakujulikana kwao. Hata walipomkataza, Yesu alisema: *"Msimkataze. Kwa maana hakuna mtu atakayefanya muujiza kwa jina langu aweze mara moja kusema vibaya juu yangu."*

Wengi hudhani kuwa hili linahalalisha miujiza yote inayofanywa leo. Sivyo ilivyo. Yesu mwenyewe alituonya:*"Kwa maana watatokea makristo wa uongo, na manabii wa uongo, nao watafanya ishara kubwa na maajabu, wapate kuwapoteza, kama yamkini, hata wale wateule. Angalieni, nimekwisha kuwaonya mbele."*(Mathayo 24:24,25)

Yesu alionya juu ya mfumo wa Mpinga Kristo ambao ungekua katika kipindi cha Injili, ambao ungefanya miujiza kwa "jina la Yesu" na kuwadanganya wengi. *"WaKristo wa uongo"* ni mifumo ya makanisa ya uongo; *"manabii wa uongo"* ni walimu wa uongo ndani ya mifumo hiyo.

Nani anayefanya miujiza hii "kwa jina la Yesu"? Paulo anatufundisha: *"Shetani mwenyewe hujigeuza awe mfano wa malaika wa nuru."* (2 Wakorintho 11:14)

Shetani hufanya miujiza hii kwa kujigeuza kuwa *"malaika wa nuru"*; huwa *"Yesu mwingine"* (2 Wakorintho 11:4). Wakristo hudanganyika na kudhani ni *"mapenzi ya Mungu"* kwa sababu ya ukosefu kamili wa maarifa ya Neno la Mungu, yaani Biblia: *"Watu wangu wameangamizwa kwa kukosa maarifa."*(Hosea 4:6)

Ukweli huu unathibitishwa zaidi:*"Yule mwovu atakuja kwa kuweza kwake Shetani, kwa uwezo wote, na ishara na maajabu ya uongo."* (2 Wathesalonike 2:9)

Kinachofanya miujiza hii kuwa ya uongo ni matumizi ya jina la Yesu huku kazi yenyewe haijaidhinishwa na Yesu kabisa.

Tuendelee kusoma:*"Na katika udanganyifu wo wote wa udhalimu kwa hao wanaopotea; kwa sababu hawakukubali kuipenda ile kweli wapate kuokolewa. Kwa sababu hiyo Mungu awaletea nguvu ya upotevu, wauamini uongo."* (2 Wathesalonike 2:10,11)

Mungu anaruhusu udanganyifu huu mkubwa wa "miujiza ya uongo." Ingawa kulikuwepo na miujiza mikubwa katika kanisa la mwanzo, ilikuwa kwa muda mfupi tu kusaidia kuimarisha imani ya kanisa mpaka maandiko ya Agano Jipya yalipokamilika. Baada ya hapo, miujiza na uponyaji hivyo vilikoma.

**✦✦✦Kutabiri / Kutoa Unabii✦✦✦**

Katika baadhi ya makanisa, "nabii" huweza kuinuka, na kwa wakati fulani hufumba macho na kuanza kutoa "unabii." Huenda akatabiri mambo ya siku zijazo kama ndoa, kuzaliwa kwa watoto, au hata vifo. Anaweza kutaja magonjwa na kuzungumza juu ya uponyaji. Haya husemwa kuwa ni kutoka kwa Bwana.

Lakini hii siyo unabii kama ulivyoelezwa na maandiko: *"Kwa maana ushuhuda wa Yesu ndio roho ya unabii."*(Ufunuo 19:10)

Yesu alifafanua maana yake kwa kusema:*"Akaanza kutoka Musa na manabii wote, akawaeleza katika maandiko yote mambo yaliyomhusu yeye mwenyewe."*(Luka 24:27)



Kama Yesu alivyowaambia wale

wawili waliokuwa katika njia ya kwenda Emau, *"maandiko yaliyomhusu yeye mwenyewe"* yalianza "kwa Musa" na kuendelea kwa *"manabii wote."* Neno "Musa" linahusu vitabu vitano vya kwanza vya Biblia: Mwanzo, Kutoka, Mambo ya Walawi, Hesabu na Kumbukumbu la Torati. "Ushuhuda wa Yesu" huu unaanzia mwanzoni mwa Biblia ambapo Mungu alisema: *"Na tufanye mtu kwa sura yetu."*(Mwanzo 1:26) — huu ni ushahidi wa Mungu akizungumza na Yesu, mshirika katika kazi ya uumbaji *(angalia Mithali 8:30)*.

Zaidi ya hapo tunasoma kuwa Mungu alizungumza juu ya "malaika" ambaye angewatangulia Waisraeli katika safari yao jangwani: *"Tazama, namtuma malaika mbele yako, ili akulinde njiani, na kukupeleka mpaka mahali pale nilipokuwekea tayari. Mwekeni sana, isikilizeni sauti yake, wala msimwasi; maana hatasamehe makosa yenu; kwa maana jina langu limo ndani yake."*(Kutoka 23:20-21)

Tunatambua kwamba "malaika" huyu hakuwa mwingine bali ni Yesu Kristo Bwana wetu*(angalia 1 Wakorintho 10:4)*.Mwisho wa Biblia tunasoma:*"Roho na bibi-arusi wasema, Njoo."* (Ufunuo 22:17) Hii inamhusu kanisa lililotukuzwa pamoja na kichwa chao na mfalme wao, Yesu Kristo.



Biblia yote ni "ushuhuda wa Yesu" kama *"mtumishi*

*wa Mungu"* aliyeinuliwa *(angalia Isaya 52:13)*na mtendaji wa Mpango wa Mungu wa Kimungu.

Kwa hiyo, **kutoa unabii wa kweli** ni kufundisha Biblia na kufunua kweli zake.

Petro alinukuu nabii Yoeli siku ya Pentekoste aliposema: *"Na juu ya watumishi wangu, waume kwa wake, nitamimina Roho yangu siku zile, nao watatoa unabii."*(Matendo 2:18)

Ni kwa **Roho Mtakatifu** tu ndipo kweli ya Mpango wa Mungu inaweza kufahamika kutoka katika maandiko na kufafanuliwa:

*"Basi mwanadamu wa tabia ya asili hayapokei mambo ya Roho wa Mungu; maana kwake huyo ni upuzi; wala hawezi kuyaelewa, kwa kuwa yatambulikana kwa jinsi ya rohoni."*(1 Wakorintho 2:14)

Biblia pia inazungumza juu ya manabii wa uongo na waalimu wa uongo:

*"Lakini palikuwapo pia manabii wa uongo katika watu, kama vile kutakavyokuwako waalimu wa uongo kwenu ninyi pia, ambao kwa hila wataingiza bidii za uharibifu hata kumkana Bwana aliyewanunua, wakijiletea uharibifu wa haraka. Na wengi wataifuata tabia yao ya upotovu; na kwa sababu yao, njia ya kweli itatukanwa. Na kwa kutamani watakufaidia kwa maneno ya kujipatia; hukumu yao tangu zamani haikawi, wala uharibifu wao hausinzi."*(2 Petro 2:1-3)

Mtume Yohana anatufundisha jinsi ya kuwatambua manabii wa uongo na waalimu wa uongo ndani ya kanisa: *"Wapenzi, msiamini kila roho, bali zijaribuni zile roho, kwamba zimetokana na Mungu; kwa sababu manabii wa uongo wametokea duniani."* (1 Yohana 4:1)

Yohana anaposema "roho," anamaanisha nini?

Katika Biblia, neno “roho” linamaanisha kitu kisichoonekana na chenye nguvu. Lina maana tatu:

1. **“Pumzi ya uhai”** *(Mhubiri 12:7)*
2. **“Akili” au “nia” ya mtu** *(Danieli 2:1)*
3. **“Maneno” au mafundisho**, kama Yesu alivyosema: *“Maneno hayo niliyowaambia ni roho, tena ni uzima.”* (Yohana 6:63)

Kwa hivyo, kama alivyoandika Yohana, “roho” humaanisha mafundisho au maneno. Kwa hiyo, kanisa linaonywa “zijaribuni roho,” linapewa agizo la kujaribu na kuchunguza mafundisho yote, ili kujua kama yametoka kwa Mungu na Neno lake. Kanisa limeambiwa *“msiamini kila roho.”* Tunapaswa kuchunguza kila kitu ili kuthibitisha kama ni kweli.

Ndivyo walivyokuwa baadhi ya Wakristo wa kanisa la mwanzo: *“Watu hawa wa Beroya walikuwa waungwana zaidi kuliko wale wa Thesalonike, kwa kuwa walilipokea lile neno kwa utayari wote, wakayachunguza maandiko kila siku, wakiangalia kwamba hayo waliyoambiwa ni kweli.”* (Matendo 17:11)

Tukiwa kama Waberoya hawa, hatutadanganywa na manabii wa uongo, kwa kuwa tutawatambua manabii wa kweli wa Mungu kupitia Neno la Mungu.

Tunasoma juu ya “nabii wa uongo” katika kitabu cha Ufunuo:*“Nikaona roho wachafu watatu, mfano wa vyura, wakitoka katika kinywa cha yule joka, na katika kinywa cha yule mnyama, na katika kinywa cha yule nabii wa uongo.”*(Ufunuo 16:13)

*“Na yule mnyama alikamatwa, na pamoja naye yule nabii wa uongo, aliyekuwa akifanya mbele yake hizo ishara, ambazo kwa hizo aliwadanganya*

*wale waliokuwa wamepokea chapa ya yule mnyama, na hao waliokuwa wakisujudia sanamu yake; hawa wawili walitupwa hai katika lile ziwa la moto liwakalo kwa kiberiti."*(Ufunuo 19:20)

Huyu "nabii wa uongo" anawakilisha mfumo unaodai kufundisha mafundisho ya Biblia, lakini hauyafundishi. Tunaamini kwamba mfumo huu ni picha ya **Shirikisho la Makanisa ya Kipentekoste na ya Kiprotestanti**. Mfumo huu wa makanisa na "unabii wao wa uongo" unaelezewa na Mungu kupitia nabii Yeremia:

*"Sikuwatuma manabii hao, walakini walikimbia; sikusema nao, walakini walitabiri."*(Yeremia 23:21)

Hawa si watumishi wa Bwana wala wa kweli yake, lakini wanaendelea kuhubiri Biblia kwenye mikutano, maeneo ya wazi, redio, na runinga.

Yeremia anaendelea kusema:

*"Bwana wa majeshi asema hivi, Msisikilize maneno ya manabii wanaowatabiria; huwafundisha ubatili; huwanena maono ya mioyo yao wenyewe, wala si kutoka kinywa cha Bwana. Huwaambia daima wale wanidharauo, Bwana asema, Mta kuwa na amani; na kila mmoja aendaye kwa ukaidi wa moyo wake, humwambia, Hakuna uovu utakaowapata. … Basi Bwana asema hivi, Tazama, mimi ni juu ya manabii wawaibao maneno yangu kila mtu kwa jirani yake. Tazama, mimi ni juu ya manabii watumiao ndimi zao, nao husema, Asema Bwana. Tazama, mimi ni juu yao watoao ndoto za uongo, asema Bwana, nao wazisimulia, na kuwapoteza watu wangu kwa uongo wao, na kwa majivuno yao; wala mimi sikuwatuma, wala sikuwapa amri; wala hawatamnufaisha watu hawa hata kidogo, asema Bwana."*(Yeremia 23:16,17,30-32)

Manabii hawa wa uongo hudai kuwa wanasema *"kutoka kinywa cha Bwana,"* lakini kwa kweli wanasema *"maono kutoka mioyo yao*

*wenyewe."* Wahubiri kwenye runinga, redio, machapisho, na kwenye mikutano hudai, *"Bwana aliniambia hivi,"* na *"Bwana alinionyesha kile."*

Hii ndiyo hukumu ya mwisho juu ya manabii hawa wa uongo: *"Nami nitawaletea aibu ya milele, na fedheha ya milele, ambayo haitasahauliwa."*(Yeremia 23:40)

*Na itakuwa siku ile, manabii wote wataona haya kwa sababu ya maono yao walipotabiri; wala hawatavalia vazi la manyoya ili kudanganya; lakini atasema, Mimi si nabii; mimi ni mkulima; maana nimekuwa mtumwa wa ardhi tangu ujana wangu. Na mtu atamwuliza, Majeruhi haya yaliyo kati ya mikono yako ni nini? Atajibu, Hayo ni majeraha niliyopigwa nyumbani kwa rafiki zangu."*(Zekaria 13:4-6)

Unabii huu wa ajabu unaelezea siku ambapo hawa manabii wa uongo watawekwa wazi. Kauli *"Mimi si nabii; mimi ni mkulima"* inaonyesha utambuzi utakaoifikia mioyo ya wale wote waliodai kuwa "walimu" na "manabii" wa Neno la Mungu. Wataelewa kuwa walikuwa wa kidunia na wa mwilini, si wa rohoni hata kidogo. Kama vile mkulima hupanda mbegu na kutafuta mavuno ya ardhini, ndivyo "manabii" hawa walivyoanzisha "huduma" kwa ajili ya kupata faida za kidunia na mali, yote kwa jina la *"huduma kwa Bwana."* Ndipo watakapoikiri kwa unyenyekevu: *"Mimi si nabii."*

Kauli *"ardhi imenilisha tangu ujana wangu"* inaashiria kukiri kwao kwamba waliwahi kufundishwa na *"mtu wa uasi wa sheria,"* yaani mifumo ya makanisa ya Mpinga Kristo na vyuo vya Biblia vya uongo ambapo kipaumbele huwekwa katika jinsi ya kuendesha huduma na makanisa—mafunzo juu ya usimamizi wa kifedha na kiutawala, si juu ya kweli ya kiroho ya Neno la Mungu. Watakiri kuwa hawakuwa wa kiroho hata kidogo.

Kauli *"majeraha niliyopigwa nyumbani kwa rafiki zangu"* inaashiria hukumu kali itakayowapata hawa "manabii" na "walimu" kutoka

kwa "rafiki" zao, wale waliowahi kuwaunga mkono na kuwaheshimu. Itakuwa ni mwisho wa kutisha kwa mifumo hii ya uongo na manabii wao wa uongo.

### ✦✦✦Maono✦✦✦

Maono ni taswira za kiroho zinazotumiwa na Mungu kueleza dhana fulani za kiroho. Mfano mmoja ni kugeuka sura kwa Yesu: *(Mathayo 17:1-9)* Petro alipata maono: *"Akaona mbingu zimefunguka, kitu kama shuka kubwa ikishushwa kwa pembe zake nne juu ya nchi; ndani yake mlikuwamo aina zote za wanyama wenye miguu minne, na vitambaavyo, na ndege wa angani. Kisha sauti ikamwambia, Simama, Petro, uchinje ule. Lakini Petro akasema, Hasha, Bwana, kwa maana sijakula kamwe kilicho najisi wala kichafu. Sauti ikamwambia mara ya pili, Vyote alivyovitakasa Mungu, usiviite wewe najisi. Jambo hilo lilitendeka mara tatu; kisha kile chombo kikapandishwa tena mbinguni."*(Matendo 10:11-16)

Maono mengi yameandikwa katika Agano la Kale na Jipya. Leo hii maono huaminika kuwa ni matukio ya kuona Yesu, au kukutana na Roho Mtakatifu kama mtu, au kuchukuliwa hadi mbinguni.

**1. Maono ya Yesu**

Hili lilimpata Sauli alipokuwa njiani kwenda Damasko: *"Akasema, Wewe ni nani, Bwana? Akasema, Mimi ni Yesu unayeniteseа. Lakini simama, uingie mjini, nawe utaambiwa yakupasayo kutenda. Wale watu waliokuwa wakisafiri pamoja naye walisimama wakiwa wamefadhaika, wakisikia ile sauti, wasimwone mtu ye yote. Sauli akaondoka, na alipofumbua macho yake hakuona cho chote; basi wakamwongoza kwa mkono mpaka Damasko. Akawa siku tatu haoni, wala hakula wala kunywa."* (Matendo 9:5-9)

Sauli wa Tarso alimuona Bwana Yesu akiwa ametukuzwa, na akapofuka; hakula wala kunywa kwa siku tatu. Baadaye aliandika: *"Mchana wa adhuhuri, Ee mfalme, nikiwa njiani, naliona nuru kutoka mbinguni, ikizidi mwangaza wa jua, ikining'aa mimi na wenzangu waliokuwa pamoja nami."*(Matendo 26:13)

Ufunuo wa Bwana Yesu ulikuwa mkali kuliko jua la adhuhuri. Ikiwa hii ndiyo hali iliyompata mtumishi mkubwa kama Paulo, kwa nini leo wahubiri wanadai kuona maono ya Yesu mara kwa mara, lakini bado wanabaki na macho yao yakiwa mazima?

**2. Maono ya Kukutana na Roho Mtakatifu Kama Mtu**

Yesu alisema kuhusu Roho Mtakatifu: *"Na tazama, nawatumia ahadi ya Baba yangu; lakini kaeni mjini mpaka mtakapopewa nguvu itokayo juu."*(Luka 24:49)

Roho Mtakatifu ni *"nguvu itokayo juu,"* ni nguvu isiyoonekana na isiyo na mipaka ya Mungu. Siyo mtu kama inavyofundishwa katika fundisho la "Utatu," ambalo ni *"fundisho la mapepo."*(1 Timotheo 4:1)

**3. Maono ya Kuchukuliwa Hadi Mbinguni**

Paulo aliandika:*"Ndugu zangu, nasema hivi, ya kuwa mwili na damu hawawezi kuurithi ufalme wa Mungu."*(1 Wakorintho 15:50)

Hakuna mtu aliye katika mwili wa kibinadamu anayeweza kuingia mbinguni. Lakini wengine hudai kuwa Paulo alichukuliwa, kwa sababu aliandika: *"Najua habari za mtu mmoja ndani ya Kristo, miaka kumi na minne iliyopita (ikiwa katika mwili sijui, au ikiwa nje ya mwili sijui, Mungu ajuaye), mtu huyo alinyakuliwa mpaka mbingu ya tatu."* (2 Wakorintho 12:2)

Hili huchukuliwa kuhalalisha uzoefu wa "kuchukuliwa mbinguni." Lakini fahamu kuwa "mbingu ya tatu" imeelezwa kuwa ni *"pepo"*


(aya ya 4), ile ile *"pepo"* ambayo Yesu alimwahidi yule mwizi msalabani: *"Akamwambia, Amin, nakuambia leo hivi, utakuwa pamoja nami peponi."*(Luka 23:43)

"Pepo" hii ni **ufalme wa Mungu**, dunia inayokuja, *"maskani ya haki."* (2 Petro 3:13)

Yeremia alizungumza juu ya mafundisho haya ya uongo: *"Bwana akaniambia, Manabii wanatabiri uongo kwa jina langu; sikuwatuma, wala sikuwaamuru, wala sikuwaambia; wanawatabiria ninyi maono ya uongo, na uganga, na ubatili, na udanganyifu wa mioyo yao."*(Yeremia 14:14)

Tunamshukuru sana Bwana kwa ajili ya kweli yake — kwa kuwa kweli hiyo imetuweka huru.

**=✿=✿=✿=Amina=✿=✿=✿=**



*Kwa Masomo zaidi Tuandikie Ujumbe kupitia:*

*Email: thekingdom1_6@gmail.com au isayaruhala25@gmail.com*

*©HAKIUZWI*

***Namba ya Whatsap: 0752965019/ +255 757 411 482***